

Nyumba ya mbuzi

Nyumba ya kawaida tu inayotengenezwa kutokana na asilia zinazopatikana katika mazingira yako inapendekezwa ili kuokoa gharama.



Nyumba ya mbuzi

Nyumba za watoto zinabadilika kutegemea mahali husika. Vibanda vya kati ya mita 1.8 na vya urefu wa mita 1.2 vinaweza kuwekwa watoto 10. Watoto wa kume wanaweza kuwekwa katika vibanda vya kipimo cha mita 2.4 kwa 1.8.

Utunzaji wa afya

Magonjwa na wadudu wa magonjwa husababisha kupotea kwa maziwa na kiwango chake pia. Pia huchangia vifo vya mbuzi. Magonjwa makuu ya mbuzi ni:

- Ugonjwa wa kuambukizana
- Ugonjwa wa matiti-hupelekea kuavya mimba
- Ugonjwa wa kuoza nyayo
- Ugonjwa wa damu
- Ugonjwa wa kulemaza
- *Coccidiosis*
- Ugonjwa wa kuambukiza wa nimonia.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Barua pepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Otieno, K

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kibos


S.L.P. 1490, KISUMU

Simu/Nukulishi: +2543544401

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 68 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Ufugaji wa mbuzi wa maziwa



Utangulizi

Ufugaji wa mbuzi wa maziwa unaendelea kutia fora hasa katika sehemu zenye uwezo pale ambapo mashamba ya kulishia ng'ombe wa maziwa yanapunguka. Sawa na ng'ombe wa maziwa hata mbuzi wa maziwa huhitaji utunzaji mwema.

Aina za mbuzi wa maziwa

Aina zinazopendekezwa ni pamoja na:

- *Anglo-nubian*
- *Toggenburg*
- *Alpines*
- *Saanen*.



Mbuzi wa kike wa Alpine

Utunzaji wa kizazi

Mbuzi wa kike anastahili kupewa mbegu ya uzalishaji akiwa na umri wa miezi 12 ili azae akiwa wa umri miezi 18. Mbegu inastahili

kutungwa masaa 12 baada ya dalili za joto kutambuliwa. Kiwango cha juu cha uzalishaji wa mbuzi hufikiwa kati ya miaka 5 hadi 6 na hata utoaji wa maziwa ni vivyo hivyo.

Chakula kwa mbuzi anayenyonyesha

Mbuzi anayenyonyesha anastahili kupewa chakula kizuri hasa katika miezi 3 ya kwanza baada ya kuzaa.

Chakula hicho kinastahili kubadilishwa ili kutia hamu ya kula kingi. Aidha chakula kingi wakati anapokuwa mja mzito hupelekea kula chakula kingi baada ya kuzaa.

Virutubishi katika chakula viongezewe katika majuma 4 hadi 6 ya mwaanzo baada ya kuzaa lakini visizidi nusu kilo.

Matatizo ya uzalishaji

Mbuzi anaweza kuavya mimba haraka zaidi kuliko wanyama wengine wowote wa kufugwa. Mara nyingi mimba hupotea kati ya siku 90-110 za kipindi cha uja- uzito kutokana na mfadhaiko. Kuavya mimba huko kunaweza kudhibitiwa

kwa lishe bora na utunzaji mwema. Aidha kwa kuchagua mbuzi hitaji la virutubishi sawa na mazingira yake.

Kuwatunza watoto wa mbuzi

Wape maziwa ya mwanzo watoto wa mbuzi siku 3 za mwanzo baada ya kuzaliwa. Hii huyasisimua matumbo ya mbuzi mtoto na kumpa vitamini iliyo na vikinga mwili inavyoweza kumpa uwezo wa kujikinga kutokana na magonjwa.

Baada ya siku 3 au 4 mpe lita 0.7 hadi 0.9 za maziwa au kibandala cha maziwa kila siku. Tumia chupa au sufuria. Mpe maziwa haya kamili mara 3 hadi 5 kila siku.

Kwa mbuzi wa maziwa kuna haja ya kuwaachisha watoto maziwa mapema ili yapatikane ya kutumiwa nyumbani. Mtoto anaweza kuachishwa kunywa maziwa ya mama akiwa wa miezi 3 bila ya kutumia vibadala vingine. Watoto wa kike wapatiwe lita moja ya maziwa kila siku nao wa kiume wapewe lita 1.5 kila siku.

Watoto wa kiume wasio wa kuzalisha wahasiriwe muda mfupi baada ya kuzaliwa kwa kutumia mpira au ala nyingine.